MINISTRY OF DEFENCE AND NATIONAL SERVICES

FORM FOUR MILITARY PRE-NATIONAL EXAMINATION.

MWONGOZO WA USAHIHISHAJI WA MTIHANI WA KISWAHILI KIDATO CHA NNE - 2026.

## SEHEMU A: (ALAMA 16)

1.

| SEHEMU A | (i) | (ii) | (iii) | (iv) | (v) | (vi) | (vii) | (viii) | (ix) | (x) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| SEHEMU B | A | C | A | D | D | C | E | A | A | A |

= Alama 1@1x10 = 10

2.

| (i) | (ii) | (iii) | (iv) | (v) | (vi) |
|---|---|---|---|---|---|
| C | I | A | B | E | D |

= Alama 1@1x6 = 6.

## SEHEMU B: (ALAMA 54)

3(a) Mtahiniwa anatakiwa kuandika nahau zenye maana sawa na tungo alizopewa.

(i) Ana mkono wa birika

(ii) Ana mkono mrefu.

(iii) Amevaa miwani

(iv) Domo kaya

(v) Piga moyo konde.

Alama = 1@1x5 = 5.

3(b) Mtahiniwa anatakiwa azingatie makosa ya kisarufi ambayo ni:-

(i) Kosa la kimsamiati: Mfano: Mbuzi wangu ameibiwa.

(ii) Kosa la kimatamshi: Mfano: Twende tukarare.

(iii) Kosa la kimuundo: Mfano: ~~Mtoto~~ Mzuri mtoto vizuri anakula

(iv) Kosa la kuongeza vitamkwa: Mfano: Nakupendaga.

(v) Kosa la kupunguza/kuacha vitamkwa. Mfano Baba ameondoka kazini.

Alama = 1@1x4 = 4

4. Mtahiniwa aeleze Changamoto Sita (6) zilizojitokeza kwa asasi, vyama na taasisi za ukuzaji wa Lugha ya Kiswahili.

CHANGAMOTO:

(i) Uhaba wa fedha za kuendeshea tafiti mbalimbali zinazohusu Lugha ya Kiswahili.

(ii) Kasumba mbaya ya jamii kuhusu kudharau Lugha ya Kiswahili.

(iii) Ukosefu wa umoja na mshikamano baina ya vyama, asasi na taasisi za ukuzaji wa Kiswahili.

(iv) Uhaba wa wataalamu wa lugha ya Kiswahili

(v) Uhaba wa vitendea kazi vya kisasa katika kuendesha shughuli za ukuzaji wa Kiswahili.

(vi) Kukosekana kwa sera za lugha ya taifa.

= Alama 1½ @1×6 = 9

5@ Mtahiniwa anatakiwa kueleza sababu za utata katika sentensi alizopewa.

(i) Kicheko amegata jiko:-

⇒ Sababu ya utata ni kutumia lugha ya picha.

(ii) Ana alimpikia:-

⇒ Sababu ya utata ni matumizi ya kauli za kutendea.

(iii) Mama Musa amefika:-


⇒ Sababu ya utata ni kutozingatia taratibu za uandishi.

(iv) Baba alileta tai:-

⇒ Sababu za utata ni kutumia neno lenye maana zaidi ya moja.

= Alama 1@1×4 = 4

5(b) Mtahiniwa anatakiwa kuchanganua sentensi kwa kuzingatia mkabala wa kimuundo.




Mtahiniwa apewe alama 1@1x5 = 5.

6. Mtahiniwa atumie tamthiliya ya Kilio chetu kueleza vyanzo sita (6) vya mmomonyoko wa maadili kwa jamii.

VYANZO VYA MMOMONYOKO WA MAADILI

(i) Utandawazi – Joti, Suzi, Mwarami, Jumbe na wengine
(ii) Ukosefu wa elimu ya kijinsia – Joti na Suzi
(iii). Malezi duni – Suzi na Joti.
(iv) Imani potofu – Mama Suzi
(v) Mapenzi katika umri mdogo – Joti na Suzi
(vi) Makundi rika
(vii) Tamaa mbaya ya vitu – Suzi

= Alama 1½ @1x6 = 9

7. Mtahiniwa anatakiwa kuandika risala kwa kufuata muundo ~~wa~~ sahihi kama:-

(i) Kichwa cha risala – kiandikwe kwa herufi kubwa, kipigiwe mstari, kutaja lengo, walengwa. = (Alama (01)
(ii) Utangulizi wa risala = (Alama 1½)

7. (iii) Kiini cha risala = (Alama 05)

(iv) Mwisho/hitimisho la risala = (Alama 1½)

Jumla = alama 09.

8. Mtahiniwa anatakiwa asome utanzu kisha ajibu maswali yanayofuata baada ya utanzu huo.

(a) Kichwa cha utanzu huo ni:-

MAZINGIRA, UMUHIMU WA MAZINGIRA, TUTUNZE MAZINGIRA (Alama 1½)

NB/ Kiandikwe kwa herufi kubwa.

(b) Dhamira ya utanzu huo ni umuhimu wa kutunza mazingira. (Alama 1½)

(c) Maana ya maneno yaliyokolezwa wino.

(i) Waja – Ni binadamu au watu. – (Alama 01)

(ii) Auni – Ni uwezo wa kufanya jambo – (Alama 01)

(iii) Dira – Ni uelekeo au mstakabali wa jambo – (01)

(iv) Mbadala – Jambo lingine, mpango mwingine au chanzo kingine – (Alama 01)

(d) Aina ya utanzu ni tenzi – (Alama 01)

Sababu – Huanza na dua/maombi maalumu

– Huwa na mishororo mstari/kipande kimoja

– Kuzingatia urari wa vina na mizani.

– Huwa na mizani nane tu.

Sababu mojawapo apewe alama (01)

Jumla = (Alama 09)

SEHEMU C: (Alama 30)

9. Mtahiniwa aeleze namna waandishi wa diwani mbili walivyotumia kipengele cha taswira kati ka kazi zao kufikisha ujumbe na hoja tatu (3) kila diwani.

9. - Kabla ya kuonesha taswira mtahiniwa atafsiri maana ya taswira katika utangulizi wake.

KIINI

- DIWANI YA WASAKATONGE:

(i) Taswira ya vinyonga kupitia shairi la "VINYONGA" yenye maana ya watu vigeugeu.
Ujumbe - Ahadi ni deni mfano ahadi za viongozi kipindi cha kampeni.

(ii) Taswira ya "Miamba" katika shairi la "MIAMBA" yenye maana ya watawala au watu wa tabaka la juu/wenye uwezo mkubwa.
Ujumbe - Ubabe na uonevu havina nafasi katika jamii yoyote ile.

(iii) Taswira ya "bundi" katika shairi la "BUNDI" yenye maana ya ukandamizaji.
Ujumbe - Ushirikiano ni chanzo cha maendeleo duni.

(iv) Taswira ya "jiko" katika shairi la "WEWE JIKO LA SHAMBA" ikimaanisha tabia ya umalaya kwa wanawake. Ujumbe - Umalaya ni chanzo cha maambukizi na ongezeko la ukimwi katika jamii.

DIWANI YA MALENGA WAPYA

(i) Taswira ya "ua" katika shairi la "UA" ikimaanisha msichana mrembo.
Ujumbe - Kizuri chajiuza kibaya chajitembeza.

(ii) Taswira ya "paka shume" katika shairi la "KWA NINI?" ikimaanisha mwanaume mwenye tabia ya uhuni
= Ujumbe - Umalaya hupelekea kutowajibika ipasavyo katika familia.

(iii) Taswira ya "njiwa" katika shairi la "NIPATE WAPI MWINGINE?" ikimaanisha mwanamke.
Ujumbe - Kuondokewa na mtu umpendaye huleta huzuni.

# DIWANI YA MASHAIRI YA CHEKACHEKA

(i) Taswira ya "Kunguni" katika shairi la "Tuambae Ukasuku" yenye kumaanisha tabia ya kurudia-rudia jambo lilelile.
Ujumbe. Yaliyopita si ndwele tugange yanayokuja.

(ii) Taswira ya "Chatu" ~~mmeza matonge~~ katika Shairi la "CHATU MMEZA MATONGE"

(iii) Taswira ya "Njiwa" katika shairi la "NJIWA KIUMBE MTINI" ikimaanisha mwanamke/msichana mrembo.

Ujumbe - Msimamo katika maisha huleta heshima kwa wanawake/wasichana.

Alama:
- Utangulizi = (Alama 2)
- Kiini = (Alama 12)
- Hitimisho = (Alama 1)

Jumla = (Alama 15)

10\. Mtahiniwa anatakiwa kutumia wahusika watatu (3) kutoka katika kila riwaya waliyobeba uhalisia wa maisha ya Watanzania.

UTANGULIZI

→ Mtahiniwa anatakiwa kueleza ~~maana~~ maana ya wahusika na kisha atambulishe vitabu atakavyovitumia kujibu swali (Alama 2)

KIINI

RIWAYA YA TAKADINI

(i) Mhusika Sekai - anawakilisha wanawake jasiri wasio kata tamaa, waleri wazuri na wenye upendo.

(ii) Mhusika Shingai - Anawakilisha wanawake wenye msimamo na maamuzi sahihi ya maisha

(iii) Nhamo - Anawakilisha kundi la wanaume wabako wasio na huruma, wanaopiga wake zao.

10. (IV) Mzee Makwati – Anawakilisha kundi la wanaume wanaoshikilia mila na desturi potofu.

RIWAYA WA WATOTO WA MAMA NTILIE.

1. Mama Ntilie – Anawakilisha wanawake wenye kujituma, upendo na uvumilivu.
ii. Mzee Lomolomo – Anawakilisha kundi la wanaume walevi, wavivu, wezi na wasiowajibika katika familia zao.
(iii) Askari wa jiji/Mgambo – Wanawakilisha kundi la viongozi wapenda rushwa au waonevu.

Alama
- Utangulizi (Alama 2)
- Kiini – (Alama 2x3x2=12)
- Hitimisho – (Alama 01)

Jumla = (Alama 15)

UTANGULIZI

11. Mtahiniwa anapaswa kutoa ufafanuzi kuhusu utamaduni na aoneshe kukubaliana na swali.

KIINI

⇒ Mtahiniwa aoneshe mambo ya Kiutamaduni yaliyooneshwa katika tamthiliya na yanayopaswa kutendeka katika jamii zetu hasa jamii za Kitanzania.

TAMTHILIYA YA KILIO CHETU.

(i) Wazazi kutoa elimu ya jinsia na malezi kwa watoto. Mfano! Wazazi wa Anna walitoa elimu ya jinsia na malezi kwa Anna.
(ii) Kuacha ukaidi pindi unaposhauriwa mambo ya msingi. Mfano Mama Suzi.

(iii) Kuhamasisha matumizi mazuri ya utandawazi. mfano: Joti na rafiki zake hawakuzingatia matumizi sahihi ya utandawazi

(iv) Kuacha kuendekeza mila na desturi potofu. mfano: Baba Joti na Mama Suzi.

(v) Kuwa na mapenzi ya dhati. mfano Anna alimpenda Suzi wakati wote.

(vi) Watoto/vijana kuepuka makundi rika yenye mienendo mibaya. mfano Joti na wenzake.

TAMTHILIYA YA NGOWE PENZI KITOVU CHA UZEMBE.

---

(i) Kujiepusha tabia ya kuchanga mapenzi na kazi - mfano Ngowe.

(ii) Kuacha kuendekeza visasi. mfano Balozi Ngengemkeni Mitomingi

(iii) Kuachana na mapenzi ya walit mfano Mazoea.

(iv) Kuacha kuendekeza ulevi wakati wa kazi mfano Mzee Jimbi na Kitaruhande.

(v) Kuachana na imani za kishirikina na kishirikina. Mama wa kwanza.

(vi) Kutoa elimu kuhusu umuhimu wa benki kwa wananchi wote katika jamii.

Alama — Utangulizi = (Alama 02)
Kiini = (Alama 2x3x2 = 12)
Hitimisho = (Alama 01)